

FAWAZA ZA MIKOJA NA SERIKALI ZA MILIA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

(Majlis ulimwete ya haramke kwenye Mikro nchi ya Afrika Kusini)

KOA WA MARA

Tel No. 028 2621055

No. 028 2621264

E-mail:halmashauri.bunda@gmail.com

7/2018



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji


S.L.P. 126,
BUNDA

TANGAZO TANGAZO

UTOAJI WA HUDUMA YA CHAKULA ZABUNI NAMBA LGA/065/2017/2018/NC/01

1. Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imepanga kutekeleza mradi wa utoaji wa huduma ya chakula kwa watumishi wake kupitia wabia wa utoaji wa huduma hiyo.
2. Huduma ya chakula inategemewa kutolewa ndani ya eneo la Ofisi kuu za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.
3. Ili huduma hiyo ya chakula iweze kutolewa, Halmashauri inamtafuta mtoe huduma ambaye ana uwezo wa kutoa huduma iliyo bora ndani ya eneo lililotengwa kwa ajili ya huduma hiyo.
4. Mwombaji atapaswa kujenga hema (Eneo la kuuzia na kulia chakula) ambalo sio la kudumu kwa mujibu wa mchoro ulioambatanishwa na Tangazo hili.
5. Mwombaji atapaswa kutokutumia Mkaa au Kuni katika kufanya shughuri zake za upishi na atahakikisha anakua na mfumo mzuri wa utunzaji/utirilishaji wa maji machafu na usafi kwa ujumla.
6. Mwombaji ye yote mwenye uwezo wa kuomba Zabuni hii ya utoaji wa huduma ya chakula anakaribishwa kuwasilisha ombi lake ambalo Mwombaji anapaswa kuhakikisha yafuatayo yanazingatiwa:
 - A. Awe na wapishi hodari na wenyewe uwezo wa kupika chakula bora
 - B. Awe ana sifa za kisheria za kuweza kutoa huduma hiyo, hii ikiwemo Usajiri, Leseni, TFDA certificate nk
 - C. Awe ana uwezo wa kujenga hema lisilo la kudumu
 - D. Mwombaji atamke ni gharama kiasi gani atatumia katika kufanya uwekezaji huo wa kujenga Hema.
 - E. Mwombaji atamke kiwango atakacho ilipa Halmashauri baada ya makato kwisha ya uwekezaji wa hema kwa mwezi.
 - F. Mwombaji atapaswa kuilipa Kiwango kitakachokubaliwa kila tarehe 05 ya kila mwezi.

- G. Mwombaji anaweza kutoa ushauri wa namna bora ya kuboresha eneo la kutoa huduma siku ya kutembelea eneo hilo.
 - H. Pale itakapoonekana inafaaa Halmashauri itaketi pamoja na Mtoa huduma na kufanya majadiliano pale itakapoonekana inafaa.
 - I. Mwombaji atapaswa kuandika jina lake kamili, Anwani na namba ya simu katika ombi lake.
- .
- Mwombaji atapaswa kuwasilisha ombi lake kwa lililofungwa vizuri ndani ya Bahasha kwa njia ya mkono na kuwasilishwa kwa Katibu Bodi ya Zabuni kabla ya tarehe **05/09/2018** siku ya **Jumatano** saa 4: 00 asubuhi na ufunguzi utafanyika katika ukumbi wa halmashuri mara tu baada ya muda wa upokeaji wa maombi kuisha.
 - Mwombaji anakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi ya Zabuni hii ya utoaji wa chakula.
 - Ombi litakalochelewa kuwasilishwa (Nje ya saa 4:00 asubuhi), litakalowasilishwa kwa njia ya posta, kwa njia ya kielectroniki na ambalo halitafungwa vizuri halitapokelewa kwa namna yeyote ile.
 - Mwombaji anakaribishwa kufika tarehe 20/08/2018 Ofisi ya Uhandisi kwa ajili ya kuoneshwa eneo ambalo linategemea kujengwa hema kwa lengo la kutoa huduma ya chakula na kuelekezwa juu ya namna hema hilo linavyopaswa kuwa.
 - Kutembelea eneo hilo ni muhimu ili muombaji ajue nini anaomba.
 - Halmashauri hailazimiki kumkubali Mwombaji yeyote kwa namna yeyote ile.



MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUNDA